# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA TANO

**29 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA THELATHINI NA TANO - TAREHE 29 MEI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 446 MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna Walimu wangapi wa Masomo ya Hisabati na Sayansi na kuna ziada au upungufu wa Walimu wangapi katika Shule za Msingi na Sekondari.

### 447 MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, upi mkakati wa kuzitengeneza Barabara za Mkoa wa Tanga zilizopo TARURA zilizofunguliwa kwa fedha za tozo na fedha zilizopelekwa Jimboni.

### 448 MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Jimbo la Kondoa Mjini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**449 MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, hatua gani imefikiwa kupeleka Umeme Kitongoji cha Songea Pori na Nindi vinavyopakana na Msumbiji kama ilivyoahidiwa na Serikali.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**450 MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha CBE katika Kata ya Lugalo - Kilolo.

**WIZARA YA UJENZI:**

**451 MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini TANROADS itamalizia kuweka Taa za Barabarani katikati ya Mji wa Korogwe kwenye Barabara Kuu itokayo Dar es Salaam hadi Arusha.

## WIZARA YA AFYA:

**452 MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga Tawi la Chuo cha Uuguzi na Uganga - Ukerewe.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**453 MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chakechake itatekelezwa.

## WIZARA YA MAJI:

**454 MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga Bwawa katika Kijiji cha Lukale na Mwabagimu Wilayani Meatu ili kuondakana na adha ya maji ya chumvi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **29 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA